



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**Ofisi ya Rais  
Tawala za Mikoa  
na  
Serikali za Mitaa**

**Utumishi katika  
Serikali za Mitaa**



## Yaliyomo

Uk.

|   |   |
|---|---|
| Utangulizi  | 1 |
| Matatizo ya Utumishi katika Serikali za Mitaa                                     | 2 |
| Kuajiriwa katika Serikali za Mitaa  | 2 |
| Ajira katika Serikali za Mitaa  | 3 |
| Uhaba wa watumishi  | 3 |
| Sifa anazohitaji Mtumishi wa Serikali za Mitaa                                    | 3 |
| Shabaha ya kuweka Utumishi Chini ya Halmashauri                                   | 4 |
| Matokeo yanayotarajiwa kutokana na uboreshaji wa Utumishi katika Serikali za Mtaa | 4 |
| Mafanikio yaliyopatikana  | 5 |
| Changamoto  | 5 |
| Hitimisho na matarajio  | 6 |

## Utangulizi

Ili serikali za mitaa ziweze kutekeleza majukumu yake, ikiwa ni pamoja na kutoa huduma inavyopashwa, zinahitaji kuwa na watumishi wa kutosha na wenye uwezo wa kutenda kazi, na wawe pia ni wale wanaoamini katika malengo ya kuwepo kwa Serikali za mitaa, yaani kuwatumikia wananchi kwa uadilifu, na kusimamia uendelezwaji wa dhana ya kuwashirikisha wananchi na kuwawezesha kupanga, na kutekeleza shughuli za maendeleo.

Wakati Serikali inabuni Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa, suala la hali ya watumishi ndani ya Halmashauri, lilikuwa ni miongoni mwa yale yaliyotakiwa kufanyiwa mabadiliko.

Serikali nyingi za Mitaa, siyo tu Tanzania, bali katika sehemu nyingi za dunia hujikuta zina matatizo makubwa ya kutokuwa na watumishi wenye sifa na ujuzi kutokana na maslahi duni katika Serikali hizi, na pia kushindwa kumudu ushindani na waajiri wengine. Hili Serikali ililiona na inalifanyia kazi kama mojawapo ya malengo ya uboreshaji wa Serikali za mitaa.

## Matatizo ya Utumishi katika Serikali za Mitaa

Kumekuwa, na kwa kiasi kunaendelea kuwepo, matatizo katika utumishi wa Serikali za Mitaa.

Baadhi ya matatizo hayo ni pamoja na:

- Upungufu wa watumishi wenye sifa zinazotakiwa kumudu majukumu makubwa yanayohamishiwa kwenye Serikali za mitaa na kukidhi matarajio ya wananchi. Tukitoa mfano wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, mwaka 2002 ilikuwa na jumla ya watuimishi 4287. Kati yao, 2639 walikuwa na sifa zinazohitajika, lakini 1648 (yaani asilimia 38.4%) hawakuwa na sifa. Mahitaji ya Jiji ni nini ili kujua upungufu huo?
- Upungufu wa aina hii unakuwa mkubwa zaidi katika Halmashauri za Wilaya. Ujana au kuwa mwanamke sio vigezo vya mahitaji ya watumishi.
- Wizara za kisekta kuendelea kuajiri watumishi na kuwapeleka katika Halmashauri. Utaratibu ambao husababisha matatizo ya uwajibikaji na udhibiti wa nidhamu.
- Mishahara midogo na kukosekana kwa motisha na hivyo Halmashauri kushindwa kuwavutia watumishi kujiunga na Halmashauri na waliomo kushindwa kubakia katika utumishi wa Halmashauri.
- Uwekaji mbaya wa taarifa na kumbukumbu za watumishi. Hili husababisha watumishi kupandishwa vyeo, kupata stahili mbalimbali, na hasa kulipwa mafao yao ya kustaafu.

Mpango wa uboreshaji wa Serikali za Mitaa unalenga kuyashughulikia matatizo hayo ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na uwajibikaji wa watumishi kwa Halmashauri zinazowaajiri. Maeneo ya Uboreshaji wa utumishi katika Serikali za Mitaa ni pamoja na:

- Kuandaa mifumo, kanuni na taratibu za kufanyia kazi katika Halmashauri. kusimamia watumishi, kuajiri, kuthibitisha kazini, kupandisha vyeo, kuendeleza, na kusimamia nidhamu ya watumishi.
- Kuandaa taratibu za kuanisha na kuendesha mafunzo ya muda mfupi, kati na muda mrefu kwa watumishi wa Serikali za Mitaa.

## Ajiria katika Serikali za Mitaa

Ajira katika serikali za mitaa inafuata sheria zilizowekwa. Utaratibu wa ajira katika Halmashauri ni kama ifuatavyo; Mkurugenzi wa Jiji huteuliwa na Rais wa nchi. Wakurugenzi wa Halmashauri za Manispaa, Mji na Wilaya huteuliwa na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa. Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2003. Ajira za Watumishi wengine zinafuata.

## Uhaba wa Watumishi

Uhaba wa Watumishi katika Serikali za Mitaa unaongezwa na janga la ukimwi, ambalo huwaathiri wafanyakazi wa ngazi zote. Serikali kupitia chombo chake cha TACAIDS imeliwekea mkakati tatizo hili ili watumishi walielewe vizuri na waweze kujikinga wenyewe na watu wengine kutokana na maambukizi ya gonjwa hili la hatari ambalo hadi sasa halina tiba wala kinga. Wakati TACAIDS inashughulikia suala hili kwa ujumla wake, mpango wa uboreshaji serikali za mitaa unatoa elimu ya uelewa kwa watumishi wa Serikali za mitaa katika mahali pa kazi.

## Sifa anazohitaji Mtumishi wa Serikali za Mitaa

Serikali za Mitaa za kileo zinazidi kubeba majukumu mengi. Pia matarajio ya wananchi, serikali kuu, wawekezaji, wafadhili na jumua ya kimataifa juu ya watumishi wa Serikali za Mitaa yameongezeka na kuchukua sura mpya. Hivyo mtumishi anayefaa, pamoja na kuwa na taaluma maalum, ingekuwa vema kama ana pia sifa zifuatavyo za ujumla:

Baadhi ya mambo muhimimu ambayo mtumishi wa Serikali za mitaa anatakiwa kuyajua ni pamoja na:

- Dhana ya utawala bora
- Kupiga vita umaskini
- Masuala ya jinsia
- Utunzaji na hifadhi ya mazingira
- Usimamizi na udhibiti wa masuala ya Fedha.

- Ushirikishwaji wa Sekta binafsi katikampango na utoaji huduma kwa Umma.

## Shabaha ya kuweka Utumishi Chini ya Halmashauri

Shabaha kubwa katika eneo

hili ni :

- Kuzipa halmashauri uwezo wa kuajiri, kusimamia na kuendeleza.
- Watumishi kuajiriwa kwa utaratibu wa ushindani na uwazi, na unaozingatia ustahili wa mtu;
- Halmashauri kuwa na watumishi kwa idadi na sifa zinazolingana na kazi zilizopo, kwa kuzingatia ufanisi unaofaa;
- Halmashauri kuwa na mipango ya kuwaendeleza watumishi na viongozi kwa kuwapatia fursa ya mafunzo zaidi, na kutekeleza mipango hii.

## Matokeo yanayotarajiwa kutokana na uboreshaji wa Utumishi katika Serikali za Mitaa

Matokeo muhimu yanayotarajiwa katika eneo hili ni pamoja na yafuatayo:

- Halmashauri kujijengea uwezo wa kuajiri, kuendeleza na kusimamia nidhamu ya watumishi wake, ili kuziwezesha Halmashauri kuto huduma bora kwa wananchi wake.
- Kuwa na programu za mafunzo kwa watumishi wake.
- Kuzitambua na kuziimarisha taasisi zinazotoa mafunzo ya Serikali za Mitaa, kwa muda mfupi na kwa muda mrefu.
- Kuwa na mikakati ya kuboresha aina mbalimbali za motisha kwa watumishi wa serikali za mitaa, na kuhakikisha zinawasilishwa serikali kuu kwa uamuzi.
- Halmashauri kuweza kutekeleza programu za kuinua kiwango cha uelewa na athari za UKIMWI, na hasa katika sehemu za kazi,

kwa manufaa ya watumishi wake na wananchi kwa ujumla.

## Mafanikio yaliyopatikana

- 1) Sheria ya Utumishi wa Umma No. 8 ya mwaka 2002 imerekebishwa ili kuzifanya Halmashauri kuwa mamlaka za Ajira kwa watumishi wa Halmashauri.

Yameandaliwa maadili ya watumishi wa serikali za mitaa ili kuwaongoza katika utendaji wao wa kazi .

- kutojihusisha na vitendo vyovyote vya rushwa
- Kutunza mali na rasilimali ya Halmashauri
- Kuongozwa na mising ya uwazi, uwajibikaji, na, demokrasia wakilishi na inayoshirikisha
- Kutojiingiza katika biashara au shughuli za kitaalamu zinazoweza kugongana na shughuli za kikazi alizopangiwa kwa kipindi chote cha ajira yake, na,
- Asiwe na upendeleo wa aina yoyote

Bodi za Ajira zimeundwa na zinafanya kazi katika Halmashauri zote.

Tatu, mafunzo yametolewa kwa viongozi wa kuchaguliwa ikiwa ni pamoja na wenyeviti wote wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa, na madiwani wote 3447 wa Halmashauri. Wakuu wote wa Wilaya Tanzania Bara wamepatiwa mafunzo, na maafisa watendaji wa kata (Ward Executive Officers) wote 2537; wakurugenzi wa Halmashauri 106, na yanaendelea kutolewa kwa watumishi wengine wa Halmashauri wakiwemo maafisa utumishi wa Halmashauri na na yanaendelea kutolewa kwa maafisa watendaji wa vijiji.

Uwekaji wa kumbukumbu umeboreshwa, kutokana na kutolewa mafunzo kwenye Halmashauri zote za awamu ya kwanza.

## Changamoto

Ingawa Sera ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa imeweka bayana mgawanyo wa majukumu ya kusimamia watumishi, baadhi ya Wizara za kisekta zimeendelea kuwasimamia watumishi walioko kwenye Halmashauri. Hii, pamoja



na mambo mengine, imeathiri uwajibikaji wa watumishi kwa mamlaka za ajira. Suala hili linaendelea kushughulikiwa na serikali ili uwajibikaji uwe kwenye mamlaka ya ajira.

Sheria za Serikali za mitaa za mwaka 1982 zilifanyiwa marekebisho mwaka 1999 ili kuziwezesha Halmashauri kuajiri, kuendeleza na kusimamia nidhamu za watumishi wake. Pia, Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 imefanyiwa marekebisho na sheria Na. 19 ya mwaka 2004 ili kuzipa Halmashauri madaraka yakuajiri na kusimamia watumishi wake. Hata hivyo, kutokana na marekebisho ya Sheria Na. 8 ya mwaka 2002, kuna maeneo muhimu, ikiwa ni pamoja na kanuni za utumishi za mwaka 2003 ambayo lazima yaangaliwe upya kwa lengo la kuondoa migongano iliyopo.

## Hitimisho na matarajio

Programu ya Kuboresha Serikali za Mitaa eneo la Maendeleo ya Watumishi imepata mafanikio, na sasa hivi Halmashauri zina

uwezo zaidi wa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na uadilifu zaidi tokea sera ya kuhamisha madaraka na majukumu kutoka serikali kuu kwenda serikali za mitaa mwaka 1998. Mafanikio haya yamekuja pamoja na kwamba bado upande wa sheria unazibana Halmashauri kwenye masuala ya ajira na fedha, motisha duni, kutoweza kuvutia wafanyakazi bora na pindi wanapopatikana, kuendelea kubaki katika ufumishi wa Halmashauri.

Majukumu yaliyopo mbele katika eneo hili ni pamoja na yafuatayo:

- Kuendelea kuzisaidia Serikali za Mitaa ili ziweze kuwa na uwezo wa kuajiri, kuendeleza, kuwajibisha na kusimamia watumishi wao;
- Kubuni na kuandaa programu za mafunzo kwa ajili ya viongozi na watumishi wa Halmashauri
- Kuendelea kuvisaidia vyo na taasisi kujenga uwezo zaidi wa kutoa huduma za mafunzo. Hii iambatane na kubuni aina za masomo yanayofaa, kwa muda mfupi na muda mrefu
- Kutathmini aina mbalimbali za motisha kwa ajiri ya watumishi wa Halmashauri ili ziweze kuwavutia wafanyakazi wenye sifa na staid zinazotakiwa.

- Kuwaongezea uwezo watumishi wa Halmashauri katika stadi maalum ambazo kwa sasa hivi hazipo ili waweze kutoa huduma katika maeneo yao.
- Kushikiana na Wizara za kisekta katika kuainisha na kutekeleza mifumo ya Utumishi ya Kitaifa, kama vile Utaratibu wa Upimaji wa Utendaji Kazi ulio wazi (Open Performance Appraisal System – OPRAS),
- Kushirikiana na Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS) katika kuelimisha watumishi wa Halmashauri kuhusu udhibiti wa janga la ukimwi katika sehemu zao za kazi.
- Kuendelea kuzisaidia Serikali za Mitaa kuimarisha na kuendeleza mfumo wa kuajiri kwa njia ya uwazi na ushindani

Progamu ya Uboreshaji wa Serikali za Mitaa itumie fursaz zinazojitokeza ili kuboresha hali ya utumishi. Fursa hizi ni pamoja na: (1) Maendeleo katika kurekebisha Sheria ya Utumishi wa Umma No. 8 ya mwaka 2002.

Kuna haja basi ya kuyalinda na kuyaendeleza mafanikio yaliyokwisha kupatikana, ili Serikali za Mitaa ziendelee kuwa na Watumishi wazuri, wenye ari ya kufanya kazi kuwatumikia wananchi, ili kuhakikisha utoaji wa huduma unaboreshwa.





na Serikali za Mitaa    Ofis  
zi ya Kijiji na Mtaa  
si ya Rais Tawala za  
za Miji  
Serikali za  
va Ra

**PO-RALG**  
Mlezi House  
P. O. Box 1923  
Dodoma  
Tanzania  
[www.poralg.go.tz](http://www.poralg.go.tz)